

HALMASHAURI YA WILAYA BUKOBA YAPONGEZWA KWA KUTEKELEZA KWA UBORA MIRADI YA MAENDELEO

Timu ya Wahandisi kutoka Ofisi ya Rais -TAMISEMI, Dodoma na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Kagera ikiongozwa na Mkurugenzi Msaidizi Mipango na Bajeti Ofisi ya Rais TAMISEMI ndugu Theonest Bagandanshwa wameipongeza Halmashauri ya Wilaya Bukoba kwa kujitahidi kutekeleza kwa ubora miradi ya elimu na afya iliyodhaminiwa na Serikali Kuu ndani ya Halmashauri hiyo na kwa kuwa na Idara ambazo zinafanyakazi kwa kushirikiana na kuwasihhi kuendeleza tabia hiyo ya ushirikiano kwani inasaidia sana utekelezaji wa miradi ya maendeleo kuwa rahisi.

Pongezi hizo zimekuja baada ya timu hiyo ya wahandisi kufanya ziara ya siku mbili kuanzia tarehe 13.7.2021 hadi tarehe 14.7.2021 ndani ya Halmashauri hiyo ambapo walitembelea shule nane za sekondari ambazo zimekamilisha ujenzi wa maabara za sayansi, shule saba za msingi ambazo zimejenga vyumba kumi na moja vya madarasa, majengo ya zahanati tatu ambazo ujenzi wake unaendelea na Ofisi za Makao Makuu ya Halmashauri hiyo ambazo pia ujenzi wake unaendelea. Maeneo yote haya ndio jumla ya miradi ambayo Serikali Kuu iliitengea fedha na kuiwezesha Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba kutekeleza katika mwaka wa fedha 2020/2021.

Naye Mkurugenzi Msaidizi Mipango na Bajeti wa Ofisi ya Rais TAMISEMI ndugu Theonest Bagandanshwa ambaye ndiye kiongozi wa timu hiyo ya wakaguzi, baada ya pongezi hizo alitoa rai kwa uongozi wa Halmashauri ya Wilaya Bukoba kuhakikisha maeneo yote ya taasisi zake yanapimwa ili kuepuka migogoro ya ardhi baina ya Halmashauri na wananchi wake na kupitia upya kwa kumtumia mhandisi wa Halmashauri hiyo gharama halisi zinazotosha kukamilisha ujenzi wa zahanati na kuwasilisha mapema iwezekanavyo gharama hizo katika Ofisi ya Mipango na Bajeti ya TAMISEMI, Dodoma na kutafuta vyanzo vingine vya mapato ili kufanikisha ukamilishaji wa ujenzi huo.

Pia Mkurugenzi Msaidizi huyo aliutaka uongozi wa Halmashauri Bukoba kuhamasisha wananchi kuendelea kujenga maboma katika taasisi za elimu na afya za Halmashauri hiyo ili serikali ilete fedha za kuyakamilisha lakini kabla hawajajenga maboma hayo wamshirikishe mhandisi wa Halmashauri ili awashauri na kuwapatia michoro yenye viwango ambavyo serikali inavihitaji katika majengo ya taasisi zake.

Kwa Upande wake mhandisi Ariff M.Almas kutoka TAMISEMI, Dodoma aliuarifu uongozi wa Halmashauri hiyo kwamba kwa kuwa Mkoa wa Kagera ni miongoni mwa maeneo yanayoathiriwa sana na matetemeko ya ardhi, serikali itaandaa michoro inayoendana na ujenzi wa mkoa wa Kagera ili majengo ya taasisi za serikali yatakatayokuwa yanajengwa ndani ya mkoa huu yaweze kumudu athari zinazoweza kusababishwa na matetemeko hayo ya ardhi.

Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Halmashauri ya Wilaya Bukoba ilipokea jumla ya shilingi bilioni mbili na milioni tisini mia tano sitini na tisa elfu (2,090,569,000.00/=) kutoka Serikali Kuu ili kukamilisha ujenzi wa maabara nane za sayansi katika shule za sekondari kila maabara shilingi milioni 30, vyumba kumi na moja vya madarasa katika shule za msingi kila chumba milioni kumi na mbili na laki tano (12,500,000/=), Ofisi ya Makao Makuu ya Halmashauri shilingi bilioni moja (1,000,000,000/=), zahanati tatu kila zahanati shilingi milioni hamsini (50,000,000/=) na wodi tatu katika hospitali ya Wilaya Bukoba shilingi milioni mia tano (500,000,000/=).

Na kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya Bukoba, Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani bibi Patricia Minja aliomba timu hiyo ya wakaguzi kuhakikisha michoro ambayo inaletwa kwa ajili ya ujenzi wa taasisi za serikali ije ikiwa imesainiwa ili kurahisisha ukaguzi hasa pale inapohitajika kujua ni nani walioidhinisha michoro hiyo. Kisha Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Bukoba ndugu Morega Mongate aliishukuru timu hiyo ya ukaguzi na kuahidi kutekeleza yale yote waliyoyapendekeza kwa ajili ya kuboresha zaidi miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Halmashauri hiyo.



Mwonekano wa nje na ndani wa Jengo la Maabara ya Shule ya sekondari Kemondo Kata Kemondo



Mwonekano wa nje na ndani wa chumba cha darasa Kata Kyamulaile Shule ya Msingi Rushaka "B" Kata Buhendangabo

Chumba kimoja cha darasa Shule ya Msingi Omukihisi



Mwonekano wa nje na ndani wa jengo la maabara ya sayansi la Shule ya Sekondari Bujunangoma Kata Kemondo



Mwonekano wa ndani na nje wa majengo ya maabara za sayansi Shule za Sekondari Kabugaro na Bujugo Kata Nyakato na Bujugo



Jengo la Zahanati ya Bituntu Kata Rukoma

Jengo la Zahanati Kazinga Kata Kaibanja



Jengo la Zahanati Mugajwale Kata Mugajwale na Majengo ya wodi ya wanaume, wanawake na watoto Hospitali ya Wilaya Bukoba



Ujenzi wa Ofisi za Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya Bukoba Bujunangoma Kata Kemondo